# Class 6 mid term 1 August 2021

# Kiswahili

Muda: Saa 1 Dak 40

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya uliyopewa.***

Ilikuwa siku ya ____1____ mwalimu alipoingia darasani ili kulianzisha funzo lake. Siku ____2____. kila mmoja wetu alitulia tuli _____3____ ili mwalimu atueleze mengi kuhusu msamiati wa ____4____ . Kwanza, alituambia kuwa nguo huvaliwa ili kujikinga na kujisitiri. Akaeleza kuwa ____5____ huvaa jezi na wanafunzi huvaa ____6_____. Kabla ____7____, kengele ilikilizwa. Sote ____8____ maana tulitaka kujua mengi kuhusu nguo mbalimbali.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. Jumapili jioni | B. Jumatatu asubuhi | C. Alhamisi usiku | D. Jumamosi mchana |
| 2. | A. wenyewe | B. lenyewe | C. yenyewe | D. zenyewe |
| 3. | A. kama mchanga wa baharini | B. kama tausi | C. kama chiriku | D. kama maji mtungini |
| 4. | A. sebuleni | B. shuleni | C. uwanjani | D. mavazi |
| 5. | A. wanakwaya | B. wachezaji | C. askari | D. walimu |
| 6. | A. sare | B. magwanda | C. deraya | D. kombati |
| 7. | A. hajamaliza | B. amalize | C. hajaanza | D. hajaingia |
| 8. | A. tulifurahi | B. tukapendezwa | C. tulihuzunika | D. tukachangamka |

_____9_____ letu limebarikiwa kuwa na wanyamapori mbalimbali ambao huwavutia ____10____ kuja kuwatazama. Wageni hao wanapokuja humu nchini ____11____ wao hulipa ____12____ ambazo husaidia kuendeleza miradi kama vile ____13____. Baadhi ya wanyama hao ni ____14____. Hii ndiyo maana wahenga walisema, ____15____.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 9. | A. Nchi | B. Taifa | C. Inchi | D. Bara |
| 10. | A. wananchi | B. wenyeji | C. watu | D. watalii |
| 11. | A. , | B. . | C. : | D. ? |
| 12. | A. kiingilio | B. pesa za wageni | C. pesa za kigeni | D. malipo mengi sana |
| 13. | A. kununua vyakula | B. kujenga barabara | C. kulipa karo | D. kujenga makao ya watu |
| 14. | A. nyani na punda | B. simba na farasi | C. ndovu na nyati | D. ng'ombe na nguruwe |

15. A. chelewa chelewa utapata mwana si wako
    B. mgeni njoo mwenyeji apone
    C. akili ni nywele, kila mtu ana zake
    D. safari ya kesho huandaliwa leo

***Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu swali kulingana na maagizo.***

**16.** Chagua nomino iliyo katika ngeli tofauti na nyingine.
A. Mwaka B. Mwana
C. Mwamba D. Mwanzo

**17.** Jibu maamkizi yafuatayo:
**M hali gani?**
A. M njema
B. Tu salama
C. Tu nzuri
D. M mzuri

**18.** Ni upi wingi wa:
**Nitamtembelea mpwa wangu** ?
A. Tutawatembelea wapwa wetu.
B. Tutawatembelea wapwa zetu.
C. Nitawatembelea wapwa wangu.
D. Tutamtembelea mpwa wetu.

**19.** Saa **3:45** kwa maneno ni saa
A. tatu kasorobo
B. tisa na robo
C. nne na robo
D. kumi kasorobo

**20.** Chagua sentensi ambayo **haina** kivumishi cha sifa.
A. Nitasherehekea siku ya kuzaliwa kwangu.
B. Ndama mdogo ameanguka shimoni.
C. Hufai kuyala maembe mabichi.
D. Darasa letu ni safi kuliko lenu.

**21.** Ni jozi gani inayoonyesha nomino iliyoundwa kutokana na kitenzi?

| | | |
|---|---|---|
| A. Mwalimu | - | fundisha |
| B. Lima | - | mkulima |
| C. Mtangazaji | - | matangazo |
| D. Upishi | - | pika |

**22.** Je, ni sentensi gani iliyoakifishwa ipasavyo?
A. "Imbeni pamoja," mwalimu alituambia.
B. Ulimwona Yohana darasani leo...
C. Parachichi ndilo tunda tamu zaidi
D. Ukinisaidia nitafurahi:

**23.** Zuena ni dada wa Abdallah. Abdallah amemwoa Asmini. Je, Zuena na Asmini wataitanaje?
A. Mpwa B. Shemeji
C. Wifi D. Mwanyumba

**24.** Kamilisha tashbihi ifuatayo:
**Mwalimu wetu ni mwaminifu kama**
A. jongoo B. njiwa
C. mlingoti D. mchana

**25.** Ni sentensi ipi iliyotumia kirejeshi kwa usahihi?
A. Tawi ambalo lililovunjika ni gumu.
B. Wewe ndiwe unayenipenda.
C. Sisi ndio tulilifagia darasa jana.
D. Shule ambalo lilijengwa ni lipi?

**26.** Teua sentensi iliyo na kiambishi **ki** cha udogo.
A. Kijiti kirefu kimekatwa.
B. Amekishika kisu kidogo.
C. Umebeba kitu gani?
D. Kiota cha ndege kimeharibika.

**27.** Chagua ala ya muziki inayochezwa kwa kupulizwa.
A. Ngoma B. Gita
C. Tari D. Tarumbeta

**28.** Kanusha sentensi ifuatayo:
**Shule zimefunguliwa nchini.**
A. Shule hazifunguliwi nchini.
B. Shule hazijafunguliwa nchini.
C. Shule hazitafunguliwa nchini.
D. Shule hazikufunguliwa nchini.

**29.** Tegua kitendawili hiki.
**Bi Kizee apepeta ufuta.**
A. Kope B. Mvua
C. Samaki D. Moto

**30.** Chagua sentensi sahihi kisarufi.
A. Watoto wenye waliadhibiwa ni hawa.
B. Wewe haufai kutumia dawa za kulevya.
C. Mvua ulikuwa ukinyesha usiku.
D. Pua ya mtoto inamwuma.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 hadi 40.***

Kuna michezo ya aina mbalimbali. Kwanza, kunayo michezo ya watoto na ile ya watu wazima. Michezo ya watoto hulenga kuwachangamsha, kuwapanua fikira, kuwaleta pamoja na pia kuijenga miili yao. Baadhi ya michezo ya watoto ni kama vile kibemasa ambao ni mchezo wa kujificha na kutafutana. Mchezo huu huwachangamsha sana watoto hasa pale ambapo wanaotafutwa hawapatikani kwa urahisi. Hapa, anayejificha vyema kuliko wote hujiona bingwa wa kibemasa au mwajificho.

Mchezo mwingine wa watoto ni ule wa kibafute. Watoto hufumbata viganja vyao huku wenzao wakikisia idadi ya vitu vilivyofumbatwa viganjani. Huu nao huwafurahisha watoto pale ambapo wanaotaja idadi ya vitu watakosea mara nyingi zaidi. Mtoto aliyefumbata viganja hujiona bingwa mwishowe.

Watoto wengine huchonga vijiti vidogo. Wao huvigonga kwa kutumia vijiti vikubwa ili viruke juu. Vikiruka, hugongwa kwa nguvu zaidi huku washindani wakishangiliwa kulingana na umbali wa vijiti vyao vidogo. Mchezo huu huitwa geli.Wanaoucheza mchezo huu wanapaswa kuwa makini sana kwani, katika harakati za kuvizungusha vile vijiti vikubwa, huenda wakawagonga wenzao ambao ndio mashabiki na watazamaji.

Kwa upande mwingine, kunayo michezo ya watu wazima. Hii huchezwa kwa sababu tofauti tofauti kama vile kujichangamsha au kushindana. Tofauti na michezo ya watoto ambayo, yote huweza kuchezwa na wavulana na wasichana pamoja, baadhi ya michezo ya watu wazima huchezwa na wanaume huku mingine ikichezwa na wanawake. Hata hivyo, michezo mingine ya watu wazima huweza kuchezwa na wanawake na pia wanaume, ila si pamoja.

Voliboli na kandanda ni baadhi ya michezo ambayo huweza kuchezwa na jinsia zote huku huo wa pili ukiwa ndio mchezo maarufu zaidi ulimwenguni. Voliboli pia huitwa mpira wa wavu. Huu huhusisha wachezaji sita katika kila upande. Pamoja na sheria nyinginezo, mara nyingi voliboli huchezwa kwa mikono. Kandanda au kabumbu huhusisha wachezaji kumi na mmoja katika kila upande. Mara nyingi, soka huchezwa kwa miguu.

**31.** Sentensi ya kwanza inatoa wazo gani?
A. Vikundi mbalimbali vya michezo.
B. Sheria mbalimbali za michezo.
C. Kuwapo kwa aina tofauti za michezo.
D. Kuwapo kwa vikundi tofauti vya michezo.

**32.** Kulingana na aya ya kwanza, michezo huweza kugawanywa kulingana na
A. sheria B. ugumu
C. jinsia D. umri

**33.** Michezo ya watoto **haiwezi** kuwasaidia
A. kujenga miili
B. kupanua mawazo
C. kuendeleza chuki
D. kuja pamoja

**34.** Ni michezo mingapi ya watoto iliyotajwa katika habari?
A. Minne B. Mitatu
C. Mitano D. Miwili

**35.** Kibemasa ni
A. mwajificho B. geli
C. kibafute D. voliboli

**36.** Ni kina nani hujiona mabingwa katika michezo ya watoto?
A. Wanaowatafuta wenzao waliojificha.
B. Wanaoleta ugumu fulani katika michezo hiyo.
C. Wanaokisia idadi ya vitu vilivyofumbatwa.
D. Washiriki wote katika michezo mbalimbali.

**37.** Chagua kauli **isiyo** ya kweli kulingana na kifungu.
A. Michezo ya watoto huweza kuchezwa na wavulana pamoja na wasichana.
B. Kandanda na voliboli huchezwa na jinsia zote pamoja.
C. Geli huchezwa kwa vijiti vidogo na vikubwa.
D. Mchezo wa geli huweza kusababisha maumivu kwa mashabiki

**38.** Mchezo wa wavu huwa na jumla ya wachezaji wangapi?
A. Kumi na wawili B. Ishirini na wawili
C. Sita D. Kumi na mmoja

**39.** Mchezo maarufu zaidi ulimwenguni
A. huchezwa na jinsia zote pamoja.
B. mara nyingi huchezwa kwa miguu.
C. pia huitwa voliboli
D. hauna sheria

**40.** Tunadokekezewa kuwa, mara nyingi, mikono hutumiwa kuchezea
A. kandanda B. kabumbu
C. soka D. voliboli

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 hadi 50.***

Tangu kitambo, Yuda alikuwa na mpango wa kumzuru bibi yake mzaa baba; na kweli, pindi tu shule zilipofungwa, nafasi hiyo ilijitokeza - nafasi ya kukizuru kijiji cha Jipindeni. Hakwenda Jipindeni peke yake. Alikuwa pamoja na mama na dada yake, Jerusha. Baba yao alibaki mjini, Angaza, walikokuwa wakisomea. Naye hakubaki peke yake bali alibaki na kaka yao aliyekuwa wa kwanza katika familia hiyo, Omieri.

Haja kuu ya Yuda kumzuru bibi ilikuwa ni kujifunza mengi kuhusu mambo ya shambani na kazi ya ukulima kwa jumla. Alifanya hivyo kwa sababu ndoto yake ukubwani ilikuwa kuwa mkulima hodari wa kusifika.

Kwanza, alijifunza kunyunyizia mimea maji katika msimu wa kiangazi ambapo huwa kuna jua kali bila mvua. Kwa sababu walifika Jipindeni katika msimu huo, hawakuwa na budi kwenda mtoni kila asubuhi na jioni kuteka maji ili kunyunyizia mimea michanga, yaani miche. Hili walilifanya na bibi tu.

Si hayo pekee, alijifunza kutayarisha shamba huku akiongozwa kufyeka nyasi na magugu kwa kutumia **chombo maalumu**. Hakika, aliifurahia sana kazi hiyo. Ilipoisha, bibi aliwaongoza na Jerusha hadi katika josho ambapo walimsaidia bibi kuwaelekeza mifugo humo joshoni ili wakaoshwe na kuondolewa wadudu kama vile kupe.

Siku zilipozidi kusonga, walijifunza kuchunga huko milimani. Ingawa kazi hiyo ilichosha kwa ajili ya usumbufu wa baadhi ya wanyama, hasa mbuzi, Yuda alikuwa na fahari kwani hakuwahi kuchunga. Zaidi ya hayo, alifurahia jinsi ambavyo mifugo hao walimtegea masikio alipowaita kwa majina.

**41.** Kulingana na aya ya kwanza, shule zilipofungwa, Yuda alimtembelea
A. mke wake
B. rafiki yake
C. mzazi wake
D. nyanya yake

**42.** Yuda alijifunza haya yote wapi?
A. Angaza
B. Jerusha
C. Jipindeni
D. Omieri

**43.** Familia ya kina Yuda ilikuwa na jumla ya watu wangapi?
A. Watano B. Wanne
C. Sita D. Watatu

**44.** Mwandishi ana maana gani anaposema **chombo maalumu**?
A. Msumeno
B. Fyekeo
C. Shoka
D. Sururu

**45.** Haja kubwa zaidi ya Yuda kumzuru bibi ilikuwa gani?
A. Kumjulia hali.
B. Kuwachunga mifugo.
C. Kujifunza mengi ya ukulima.
D. Kutayarisha shamba.

**46.** Kina Jerusha walifika kijijini katika majira gani?
A. Kiangazi
B. Masika
C. Vuli
D. Kipupwe

**47.** Kulingana na taarifa, mifugo huoshewa wapi?
A. Mtoni B. Mlimani
C. Joshoni D. Malishoni

**48.** Taarifa inasema kuwa mnyama msumbufu ni
A. Kondoo
B. Ng'ombe
C. Punda
D. Mbuzi

**49.** Kwa maoni yako, ni mnyama yupi hapa hakuwa milimani?
A. Ng'ombe B. Swara
C. Mbuzi D. Kondoo

**50.** Kulingana na paragrafu ya mwisho,
A. baadhi ya wanyama walikuwa na majina.
B. bibi aliwaongoza Jerusha na Yuda hadi joshoni.
C. Yuda na bibi tu ndio walioenda mtoni.
D. kaka wa Yuda alibaki mjini na baba yao.